

Uwazi katika Bajeti Yetu Je, tunasonga mbele au Kurudi Nyuma?

Utangulizi

Uwazi wa bajeti ni muhimu wa sababu huwezesha wananchi kupata taarifa ya jinsi gani serikali imepanga fedha kwa ajili ya huduma mbalimbali za jamii. Pia huchochea ushiriki wa wananchi kufahamu fedha zao zinavyopangwa na kutumika kuboresha huduma. Uwazi wa wa bajeti huboresha maisha kwa sababu huchochea uwajibikaji wa jamii na viongozi wa serikali.

HakiElimu kwa kushirikiana na Shirika la International Budget Partnership imekuwa likifanya utafiti wa kupima uwazi wa mfumo wa bajeti wa Tanzania kwa kutumia nyaraka muhimu za bajeti.

Kipimo cha Kufuatilia Uwazi wa Bajeti ni zana ya kutoa mrejesho wa namna serikali inavyoweka wazi nyaraka muhimu nane za bajeti kwa kila mwezi katika mwaka wa fedha husika kwa kila nchi. Ripoti hii inahusu takwimu zilizokusanywa kuanzia tarehe 1 Novemba mwaka 2013 hadi tarehe 30 Septemba 2014.

Nyaraka nane muhimu zinazopaswa kuwekwa wazi ni;

1. Tamko la bajeti ya wali
2. Mapendekezo ya Bajeti kuu ya serikali
3. Bajeti ya wananchi
4. Bajeti iliyopitishwa Kisheria
5. Ripoti za utekelezaji wa Bajeti za Kila Robo ya mwaka wa fedha
6. Ripoti ya utekelezaji wa Bajeti nusu mwaka wa fedha
7. Ripoti ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha
8. Ripoti ya Ukaguzi

Matokeo kwa Tanzania

Tanzania imeweka wazi nyaraka 5 kati ya nyaraka 8 kama inavyooneshwa katika jedwali namba 1.

Jedwali namba 1: Upatikanaji wa Nyaraka za Bajeti kwa Umma

Nyaraka	Mwaka wa fedha	Hali ya upatikanaji
Tamko la bajeti ya wali	2014/2015	Iliwekwa wazi
Mapendekezo ya Bajeti kuu ya Serikali	2014/2015	Iliwekwa wazi
Bajeti ya Wananchi	2013/2014	Iliwekwa wazi
Bajeti iliyopitishwa kisheria	2014/2015	Haikuwekwa wazi
Ripoti ya utekelezaji wa bajeti za kila robo ya mwaka wa fedha	2013/2014	Haikuwekwa wazi
Ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya nusu mwaka wa fedha	2013/2014	Haikuwekwa wazi
Ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya mwisho wa mwaka wa fedha	2012/2013	Iliwekwa wazi
Ripoti ya ukaguzi	2012/2013	Iliwekwa wazi

Hii ni tofauti na matokeo ya Open Budget Survey 2012 ambapo Tanzania iliweza kuweka wazi nyaraka 6 kati ya 8. Tafsiri tunayoipata hapa ni kuwa miaka ya nyuma Tanzania iliweza kuweka wazi ripoti za robo mwaka za utekelezaji kwa muda unaopaswa lakini kati ya kipindi cha Novemba 2013 hadi Jun 2014 ni ripoti moja tu ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha iliweka wazi. Ripoti hizi zinapaswa kuwekwa wazi miezi mitatu baada ya kumalizika kwa kila robo lakini Tanzania ilichelewa kuziweka wazi.

Jambo la kushangaza, kati ya nchi 30 zilizohusishwa kwenye tathmini hii, Tanzania peke yake ndio haijaweka wazi Ripoti ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha kwa muda uliotakiwa.

Tamati na Pendekezo

Hatuoni sababu kwa Tanzania kushindwa kutengeneza ama kuweka wazi hizi ripoti tatu. Jambo la msingi hapa ni nia ya dhati na utashi wa serikali kutekeleza hili hasa ukizingatia Tanzania ni moja ya nchi zinazotekeleza Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Serikali kwa Uwazi(OGP)